

**HOTUBA YA MWENYEKITI WA BODI YA WAKURUGENZI
WA MFUKO WA TAIFA WA BIMA YA AFYA, MHE. ANNE
SEMAMBA MAKINDA WAKATI WA KUPOKEA CHETI CHA
UTOAJI WA HUDUMA BORA KWA VIWANGO VYA
KIMATAIFA (ISO) TAREHE 20/08/2018**

Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia
Wazee na Watoto, Mhe. Dk. Faustin Ndungulile (Mb)

Wajumbe ya Bodi ya Wakurugenzi ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya
Afya,

Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya,

Viongozi wa Taasisi na Idara Mbalimbali mliopo hapa,

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam,

Mwakilishi kutoka BSI,

Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi,

Watumishi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya,

Wanahabari,

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, kwa niaba ya Wajumbe wa Bodi ya
Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya, napenda kumshukuru Mwenyezi
Mungu mwenye wingi wa rehema kwa kutufikisha siku ya leo
tukiwa wenye afya njema. Binafsi, nakushukuru sana Mheshimiwa

Naibu Waziri kwa kutumia muda wako adimu kuja kushiriki nasi hapa kwenye tukio hili muhimu.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Mimi pamoja na Bodi yangu tulipokabidhiwa kazi hii, jambo kubwa ambalo tuliona na kulipa kipaumbele ni pamoja na kuhakikisha Shirika letu linafikia utoaji wa huduma bora kwa viwango vya Kimataifa hivyo suala hili tuliliamua kwa dhati na kuhakikisha kwamba azma hii njema inafikiwa kwa manufaa ya wanachama wetu na wananchi kwa ujumla. Pamoja na juhudi zinazoendelea kufanywa na Bodi kuhakikisha malengo tuliyojiwekea yanakamilika, suala la kuwa na viwango vya ubora wa huduma tulilipa kipaumbele na tuliwaagiza Menejimenti ya Mfuko kuangalia njia zitakazofanikisha jambo hili kwa haraka na kwa ufanisi. Menejimenti ililichukua suala hili kwa uzito wake na kulifanyia kazi.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Tendo utakalolifanya muda mfupi ujao la kupokea cheti cha ubora wa Kimataifa baada ya Mfuko kuthitibitishwa na wenzetu ambao ndio wataalam wa usimamizi wa viwango vya Kimataifa (British Standards Institute - BSI), linaashiria mwanzo mpya wa utendaji kazi wa Mfuko ambao unakwenda sambamba na ndoto za Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Magufuli.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Kwa leo nisingependa kuzungumza mambo mengi ila nikuhakikishie tu kwamba mimi na Bodi yangu tuko imara kuhakikisha tunaisimamia vyema Menejimenti ya Mfuko katika utekelezaji wa shughuli zake ili malengo ya Serikali yaweze kufikiwa lakini pia huduma zinazotolewa zizingatie vigezo vya kimataifa ambavyo leo tunapata cheti chake.

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, Serikali yetu ina azma ya kuhakikisha kila mtanzania anakuwa na bima ya afya na huko ndiko tuendako. Ili Mfuko huu uweze kumudu kuwahudumia wananchi hawa, hatuna budi kujihakikishia tunatoa huduma katika ubora unaotakiwa. Mchakato huu wa Ubora wa Viwango vya Kimataifa vya Huduma, ni chachu kubwa katika kutufikisha huko.

Yapo mambo ambayo kama Bodi tunayaangalia kwa karibu sana na ambayo tumeiagiza Menejimenti kuyawekea mkakati wa haraka ambayo ni pamoja na:-

- **Kuhakikisha cheti hiki kinatunzwa kwa maana ya kuendelea kuboresha zaidi huduma kwa wanachama na wadau wake kwa ujumla.**

- **Utekelezaji wa utoaji wa huduma bora kwa viwango vya kimataifa ufanyike katika Ofisi zote za Mfuko Tanzania nzima na hili lianze mara tu baada ya kukamilisha awamu hii ya kwanza na kupata cheti.**
- **Kuendelea kuboresha mazingira ya utoaji wa huduma pamoja na vitendea kazi kwa watumishi ili waweze kutimiza azma hii.**

Mheshimiwa Mgeni Rasmi, nikuhakikishie kuwa yote haya yatafanyika ili Mfuko uzidi kuimarika na kuhudumia wataanzania kwa ubora zaidi nami na Bodi yangu tutaendelea kuisimamia Menejimenti ya Mfuko ili iweze kutimiza na kufikisha ndoto ya Serikali ya Awamu ya Tano ambayo imejielekeza katika kuwahudumia wananchi hususan wanyonge.

Baada ya kusema haya naomba sasa nikukaribishe Mheshimiwa Mgeni Rasmi ili uweze kusema na hadhara hii na kisha kupokea cheti.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.